JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

# TAARIFA YA MKURUGENZI MKUU MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA) ENG. BENEDICT NDOMBA KWA WAZIRI WA KILIMO MHE. HUSSEIN BASHE (MB), WAKATI WA UZINDUZI WA MFUMO WA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (MUVU) MKOANI TABORA,

**JULAI 01, 2023**

---

*Mhe. Hussein Bashe (Mb); Waziri wa Kilimo,*

*Mhe. Antony Peter Mavunde (Mb), Naibu Waziri wa Kilimo,*

*Mhe. Mariam Ditopile, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo*

*Viongozi wa CCM – Mkoa wa Tabora,*

*Mhe. Balozi Dkt. Batilda Buriani: Mkuu wa Mkoa wa Tabora,*

*Wahe. Wakuu wa Mikoa mliopo,*

*Wahe. Wakuu wa Wilaya mliopo,*

*Abdulmajid Nsekela; Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC),*

*Dkt. Benson Ndiege; Mrajisi wa Vyama vya Ushirika,*

*Zainab Hassan; Mwakilishi wa Mrajisi, Vyama vya Ushirika Zanzibar,*

*Prof. Alfred Sife; Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU)*

*Xavery Mkingule; Mtendaji Mkuu wa Shirika la Ukaguzi Vyama vya Ushirika (COWASCO),*

*Charles Jishuli: Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika,*

*Wakurugenzi wa halmashauri mbalimbali,*

*Wana ushirika,*

*Waandishi wa Habari,*

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa leo, katika hafla hii maalum ya uzinduzi wa Mfumo wa kielektroniki, wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ujulikanao kama (MUVU).

Napenda kutumia nafasi hii kukushukuru sana **Mhe. Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo,** kwa kushiriki nasi ili kuzindua mfumo huu wa MUVU. Tunafahamu kuwa, unayo majukumu mengi muhimu ya kitaifa, lakini umeona ni vema ushiriki nasi katika tukio hili muhimu. Tunakushukuru sana **Mhe. Waziri.**

Aidha, napenda kuwashukuru Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu, Viongozi wa CCM mkoa wa Tabora, Viongozi wa Mkoa wa Tabora Pamoja na mikoa jirani, Viongozi na Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Wanaushirika pamoja na Waandishi wa Habari, kwa kushiriki nasi katika hafla hii muhimu, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kukuza Serikali Mtandao.

**Mhe. Mgeni rasmi,** Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni Taasisi ya Umma yenye jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kuhimiza uzingatiwaji

wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili kuhakikisha Taasisi za Umma zinatumia TEHAMA kwa ubora, usahihi na usalama.

Katika utekelezaji wa jitihada hizo, Mamlaka hushirikiana na Taasisi nyingine za Umma, katika kusanifu na kujenga Mifumo mbalimbali ya TEHAMA, ili kurahisisha na kuboresha utendaji kazi ndani ya Taasisi hizo, pamoja na utoaji wa huduma kwa wananchi**.**

**Mhe. Mgeni rasmi,** Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) imeweza kusanifu, kutengeneza na kuendesha Mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ujulikanao kama (MUVU), unaowezesha na kurahisisha uhamasishaji, Usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kidijitali.

Mfumo huu umetengenezwa hapa nchini kwa kutumia wataalamu wazawa kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika (TCDC). Mfumo huu umejengwa kwa kutumia Teknolojia za kisasa na kwa kuzingatia mambo muhimu, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kubadilishana taarifa na mifumo mingine na usalama wa taarifa pamoja na miundombinu yake. Aidha, Mfumo huu ambao unauzindua leo kwa sasa upo kwenye hatua za majaribio, na Mamlaka ya Serikali Mtandao itaendelea kutoa ushirikiano na usimamizi wa karibu wa Mfumo huu na miundombinu yake.

**Mhe. Mgeni rasmi,** itakumbukwa kuwa, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** amekuwa akisisitiza juu ya kuimarisha Serikali ya Kidigitali ili kuboresha utendaji kazi serikalini, utoaji wa huduma bora kwa umma pamoja na kukuza uchumi wa taifa letu. Kwa kuzingatia azma hiyo, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeendelea kuweka mazingira wezeshi yanayozisaidia Taasisi za Umma, kutumia TEHAMA katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku ili kutoa huduma bora kwa Umma.

Vilevile, **Mhe. Rais** ametuelekeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kwenda sambamba na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yaliyotamalaki hivi sasa Duniani kote, ambayo yamepelekea shughuli nyingi duniani zikiwemo za kiuchumi kufanyika kwa kutumia TEHAMA yaani Uchumi wa kidigitali.

Katika kutekeleza agizo hilo, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeendelea kufanya tafiti na bunifu ili kuibua Mifumo ya TEHAMA itakayoimarisha sekta za Kilimo, Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Madini, Utalii, Afya, Elimu, Kazi na Ajira, Ustawi wa Jamii, Masuala ya Kimataifa, Nishati, Fedha na kodi, Ulinzi na Usalama, Habari na Mawasiliano, Miundombinu na Uchukuzi, Ardhi na Makazi, Mifugo, Katiba na Sheria, n.k.

**Mhe. Mgeni Rasmi,** maelekezo mengine ya Mhe. Rais ni kuwa na mifumo michache inayozungumza kwa maana ya kubadilishana taarifa. Katika kutekeleza maagizo haya, Mamlaka imesanifu na kujenga mfumo wa kuwezesha mifumo yote kubadilisha taarifa kwa usahihi, wakati na usalama ujulikanao kama *'**Government Enterprise Service Bus'*** **(GovESB).**

Aidha, katika kupunguza urudufu wa Mifumo, Mamlaka imeanza kusanifu na kujenga mifumo ya Kisekta kwa kushirikiana na Sekta husika, ambapo katika Sekta ya Maji, Mamlaka imefanikiwa kujenga mfumo wa MAJIS unaosimamia utoaji wa ankara za maji kwa Mamlaka zote za Maji nchini, na sasa Mamlaka inaendelea na zoezi hili kwenye Sekta ya Ardhi.

Lengo la ujenzi wa mifumo ya kisekta ni kupunguza uwingi na urudufu wa Mifumo ili kuongeza ufanishi, kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo ya TEHAMA na kumrahisishia Mwananchi kuhudumiwa na mifumo michache.

**Mhe. Mgeni Rasmi,** katika mwaka mpya wa fedha 2023/2024 ambao umeanza leo hii, Mamlaka imejipanga kufanya kazi katika Sekta yako ya Kilimo kwa kujenga Mfumo mkuu wa Kisekta wenye dirisha moja tu kwa Mkulima, msambazaji wa pembejeo na mfanyabishara wa Kilimo yaani ***'Agriculture Single Window'***, mifumo mingine itakuwa ni mifumo saidizi yaani '*backend supporting systems'* itakayokuwa inazungumza na mfumo mkuu wa Kilimo.

Mfumo mkuu utakuwa umebeba mnyororo mzima wa thamani wa Kilimo yaani '***Agriculture Supply Chain***'. Hivyo basi**, Mhe.Mgeni Rasmi**, naomba kutoa wito kwa wadau wa Sekta ya Kilimo kuunga mkono juhudi hizi na kutoa ushirikiano, ili Mamlaka iweze kutekeleza agizo la Mhe. Rais na sheria ya Serikali Mtandao inayoitaka Mamlaka kutengeneza mifumo michache inayowasiliana.

**Mhe. Mgeni rasmi,** Mamlaka ya Serikali Mtandao, imejipanga kufanya mageuzi katika utoaji huduma za Serikali kidigitali ili kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma, pamoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma mtandao kwa wananchi wote hususan wanaoishi vijijini. Sanjari na hilo, sisi watendaji tumedhamiria kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita za kuleta mageuzi katika utoaji wa huduma za Serikali kidigitali.

Aidha, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) itaendelea kushirikiana na Taasisi za Umma katika kuhakikisha inajenga Mifumo inayotatua changamoto tulizonazo ili kufanikisha dhana nzima ya Serikali ya kidigitali.

Baada ya kusema hayo naomba kuhitimisha kwa kukushukuru tena wewe binafsi, viongozi wakuu wa serikali, na wageni wote mliohudhuria tukio hili muhimu.

***Mungu ibariki Afrika,***

***Mungu ibariki Tanzania,***

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***